JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA
(Kimeanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura 315 Marejeo ya 2023)

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kinawatangazia wananchi wote, taasisi za umma na binafsi, makampuni, wawekezaji pamoja na wadau wengine wenye nia ya kununua ardhi kuwa, kutakuwa na mnada wa hadhara wa kiwanja kinachomilikiwa na Chuo katika Mkoa wa Mwanza.

TAARIFA ZA KIWANJA NA MNADA

MAHALI KILIPO	Kiseke, Wilaya ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza
NAMBA YA KIWANJA	Kiwanja Na. 139–142, Block D
UKUBWA WA KIWANJA	Hekta 8.112 sawa na mita za mraba 81,120(m^2)
AINA YA UUZAJI	Mnada wa hadhara
TAREHE YA MNADA	Jumamosi, tarehe 21 Novemba 2026
MUDA WA KUANZA	Saa 4:00 asubuhi
MAHALI PA MNADA	Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Kampasi ya Mwanza, Mecco Kangaye

MASHARTI YA MNADA

1. Kiwanja kitauzwa katika hali kilichonayo na mahali kilipo. Mnunuzi anashauriwa kukitembelea na kukikagua kabla ya kushiriki katika mnada.

2. Mtu, kampuni au taasisi itakayoshinda mnada itatakiwa kulipa amana isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya mauzo mara baada ya kutangazwa mshindi wa mnada.

3. Mnunuzi atatakiwa kukamilisha malipo ya kiasi kilichobaki ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya mnada.

4. Mnunuzi atakayeshindwa kulipa kiasi chote cha fedha ndani ya muda uliopangwa atapoteza haki yake ya kununua kiwanja hicho. Aidha, amana yoyote aliyokwisha kulipa haitarejeshwa.

5. Baada ya kukamilisha malipo yote, mnunuzi atatakiwa kuanza na kukamilisha taratibu za uhamisho wa umiliki wa kiwanja ndani ya siku sitini (60) tangu siku ya kukamilisha malipo.

6. Wananchi, wawekezaji na wadau wote wenye nia ya kushiriki katika mnada wataruhusiwa kukagua kiwanja siku tano (5) kabla ya tarehe ya mnada, yaani kuanzia tarehe 16 hadi 20 Novemba, 2026, kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana kila siku ya ukaguzi.

7. Gharama zote zinazohusiana na ununuzi, uhamisho wa umiliki, kodi, ada, tozo na taratibu nyingine za kisheria zitabebwa na mnunuzi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zinazotumika.

Mtaa wa Bibi Titi Mohamed, S. L. P. 1968, **Dar es Salaam**
Simu Na.: +255 22 2150177; **Nukushi Na.: +**255 22 2150122; **Barua Pepe:** rector@cbe.ac.tz; **Tovuti:** www.cbe.ac.tz

8. Chuo cha Elimu ya Biashara kinahifadhi haki ya kutoa ufafanuzi wa masharti ya mnada na kuchukua hatua zinazostahili kwa mujibu wa sheria na taratibu za mnada.

WITO KWA WAWEKEZAJI

Hii ni fursa muhimu kwa wawekezaji, taasisi, makampuni na wananchi wenye uwezo wa kuwekeza katika ardhi iliyopo katika eneo la Kiseke, Mwanza. Wenye nia wanashauriwa kufika mapema katika eneo la mnada, kusoma na kuelewa masharti yote, pamoja na kuwa tayari kutekeleza wajibu wa malipo endapo watashinda mnada.

IMETOLEWA NA:

MKUU WA CHUO

CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA

02 November,2026